# JESHI LA KUJENGA TAIFA

Simu ya Upepo: "JKT"
Simu ya Mdomo: +225-22-27582/8
Telefax: +255-22-2780048
Tovuti: www.jkt.mil.tz
E-mail: info@jkt.mil.tz

Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa
Sanduku la Posta 2963,
**Dodoma,** Tanzania
27 Mei, 2025.

## TAARIFA KWA UMMA

### WITO WA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA JKT MUJIBU WA SHERIA MWAKA 2025

Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Meja Jenerali Rajabu Nduku Mabele, anatoa wito kwa Vijana waliohitimu elimu ya sekondari kidato cha sita kwa mwaka 2025, kutoka Shule zote za Tanzania Bara kuhudhuria Mafunzo ya JKT kwa Mujibu wa Sheria kwa mwaka 2025.

Sanjari na wito huo, JKT limewapangia makambi watakayo kwenda kupatiwa Mafunzo na wanatakiwa kuripoti makambini kuanzia tarehe 28 Mei 2025 tarehe hadi 08 Juni 2025.

Vijana hao wamepangwa katika Kambi za JKT zifuatazo; JKT Rwamkoma - Mara, JKT Msange - Tabora, JKT Ruvu na JKT Kibiti - Pwani, JKT Mpwapwa, JKT Makutupora - Dodoma, JKT Mafinga –

Iringa, JKT Mlale - Ruvuma, JKT Mgambo na JKT Maramba -Tanga, JKT Makuyuni na JKT Orjolo - Arusha, JKT Bulombora, JKT Kanembwa na JKT Mtabila - Kigoma, JKT Itaka - Songwe, JKT Luwa na JKT Milundikwa – Rukwa pamoja na JKT Nachingwea – Lindi.

Wahitimu wenye ulemavu wa kuonekana kwa macho (Physical Disabilities) waripoti katika Kambi ya Ruvu JKT iliyopo Mlandizi Mkoani Pwani ambayo ina miundombinu ya kuhudumia watu wa jamii hiyo.

Aidha JKT linawataka vijana hao kuripoti wakiwa na vifaa vifuatavyo.

1. Bukta ya rangi ya 'Dark Blue' yenye mpira kiunoni (lastic), iliyo na mfuko mmoja nyuma, urefu unaoishia magotini, isiyo na zipu.
2. T-shirt ya rangi ya kijani.
3. Raba za michezo zenye rangi ya kijani au blue.
4. Shuka mbili za kulalia zenye rangi ya blue bahari.
5. Soksi ndefu za rangi nyeusi.
6. Nguo za kuzuia baridi kwa waliopangiwa mikoa yenye baridi.
7. Track suit ya rangi ya kijani au blue.
8. Nyaraka zote zinazohitajika katika Udahili wa Kujiunga na Elimu ya Juu, zikiwemo cheti vya Kuzaliwa, Vyeti vya Kuhitimu kidato cha Nne n.k
9. Nauli ya kwenda kuripoti makambini na kurudi nyumbani.

Orodha kamili ya majina ya vijana hao, Makambi ya JKT waliyopangiwa na maeneo Makambi hayo yalipo na vifaa wanavyotakiwa kwenda navyo, Inapatikana katika tovuti ya JKT ambayo ni **www.jkt.mil.tz**

Aidha, **ili kufahamu kambi kijana aliyopangiwa, atatakiwa kuingiza jina la shule au namba ya shule aliyohitimu elimu ya kidato cha sita, mbele ya jina la shule yake ataona neno lililoandikwa waliochaguliwa, akichagua neno hilo ataona jina au majina ya waliochaguliwa kujiunga na Mafunzo ya JKT kwa Mujibu wa Sheria kwa mwaka 2025, ikionesha kambi aliyopangiwa, Mkoa na Wilaya ilipo kambi hiyo.**

**Ili kuona majina yote ya vijana na kambi walizopangiwa, mtumiaji atapakua JKT PDF 2025 iliyopo juu kulia katika ukurasa huo.**

Mkuu wa JKT Meja Jenerali Rajabu Nduku Mabele, anawakaribisha vijana wote waliohitimu kidato cha sita mwaka 2025 kuungana na Vijana wenzao ili kujengewa Uzalendo, Umoja wa Kitaifa, kufundishwa stadi za kazi, Stadi za Maisha na Utayari wa Kulijenga na Kulitumikia Taifa lao.

**Imetolewa na:**
**Kurugenzi ya Habari na Uhusiano,**
**Makao Makuu ya JKT,**